



SWAHILI

**BUFFALO PUBLIC SCHOOLS**

**Office of the Superintendent**

65 Niagara Square Room #712 City Hall  
Buffalo, New York 14202

Phone (716) 816-3575 \* Fax (716) 851-3033  
krinercash@buffaloschools.org

Terehe 31, mwezi wa 8, 2021

Wazazi wapendwa na nyi wasimamizi:

Munakaribishwa kwa mwaka wa mashule wa 2021-2022!

Tunaanza kwa kumkaribisha Mheshimiwa Kathy Hochul kwa mamlaka yake mapya ya kuwa Gavana wa Serikali ya New York, na kumshukuru kwa msimamo wake imara, wa kuunga mkono usalama wa wote kwa kuamrisha kuvaa barakoa kwa mashole yote serikalini.

Tuko tayari kutia kichapuzi kwa mafunzo unawosababishwa na ugonjwa wa mlipuko wa COVID-19 duniani. majengo yetu ya mashule yako tayari. Taratibu za mafunzo na vyombo cya teknolojia viko tayari. Magari yetu ya uchukuzi yako tayari; lakini tunaomba muwe na ustahamilivu. Kilicho muhimu sana ni kuona walimu wetu pamoja na wakurugenzi wa mashule wamejitayarisha kabisa kwa sherehe hizi za watoto kurudi madarasani. Bilas haka, washirika wote wa mashule ya Serikali mjini Buffalo wako tayari kuwakaribisha na kuwahudumiya watoto wenu.

Maandalizi yetu atakuwa na mafanikiyo mapungufu kama nyinyi wazazi hamutafanya munayotarajiwa kufanya kwenu nyumbano. Tafadhali wasaidiyeni watoto wenu kupata mafanikio kamili wanayostahili, kwa kutimiza mamlaka muhimu afuatayo:

1. Iwapo mtoto ikon a afya nzuri, mufanye kuhudhuriya shule, kila siku, kwa siku mzima.
2. Mwaidie mtoto kwa kumpa mahali pa kimya nyumbani pa kufaniya mazoezi ya shule nyumbani na kujifundisha mwenyewe zaidi, hata kwa masaa mawili kila siku. Muulize mtoto wako aliyofauli kufanya shuleni kila siku na mwambiye una matarajio makubwa kwa mafanikio yake shuleni.
3. Mpangiye mtoto wako kupimwa na mganga wake. Unaweza ukapata msata wa watumishi wa mashule kwa taratibu hizi. Fanya bidhii kuhakikisha mtoto wako awe na kingamaladhi za kisasa kama vilivyoamrisha.
4. Iwapo haujapata chanjo, basi fanya haraka na kupata sindano hizi. Na wapangiye watoto wako wa miaka 12 na zaidi kupata sindano sa kinga, iwapo hawajazipata
5. Iwapo haujayirudisha, basi fanya haraka na kurudicha chombo cha kompyuta cha mtoto wako kwa anwani ya 1515 South Park Ave, Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa nne hadi saa kumi jioni, ili tuweze kuzitengeza upya na kuzirudishia wanafunzi.

Asante sana kwa kujiunga nasi kwa kutimiza jukumu yenu ya kumpa mtoto wenu elimu. Jiunge nasi tena kwa kuendelea kuwa samala, kufanya kazi vilivo, kuheshimu elimu, ana kuendelea kuwa pamoja kwa mamlaka haya kwa kizazi chetu. Tembea polepole ndani ya magari yenu. Muwe macho kwa watoto barabarani. Tuna furaha kubwa kwa matarajio ya siku ya Jumatano terehe ya 8 mwezi wa 9, tutakapokaribisha watoto wetu wakirudi madarasani waliwo subiri kwa muda mrefu!

Wenu awapendaye,

Dr. Kriner Cash

Msimamizi mkuu wa mashule

Ambatishos: Nakala ya pili ya taratibu za usalama kutoka uwongozi wa mashule  
Mkataba na Wanafunzi pamoja na Wazazi

***“Kuweka wanafunzi na familia mbele ili kuwasaidia wote kuwa na mafanikio ya hali ya juu”***